East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 2, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?

*Dr. Kibigo Mary Lukamika, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Tom Mboya, S. L. P. 199 – 40300 Homa Bay, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-5454-0123; Barua pepe ya mawasiliano: kibigomary@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*09 Novemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Matapo, Fasihi Simulizi, Usasa, Usasaleo, Ukale, Ujadi, Kiethnografia.*

**IKISIRI**

Makala hii inahusu matapo na namna yanavyojitokeza katika fasihi simulizi. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha na vitendo kuwasilisha ujumbe kuhusu maisha ya binadamu. Fasihi simulizi ndiyo fasihi mama na iliyo na historia ndefu. Hata hivyo, wataalamu wengi wamekuwa wakishughulikia dhana ya matapo katika fasihi andishi bila kuzingatia uwepo wa matapo katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Makala inalenga kuyaweka wazi matapo ya fasihi simulizi ya Kiswahili ili kubaini mchango wake katika Sanaa. Vilevile, Makala yanalenga kutathmini matapo hayo kwa kutumia mifano kutoka katika mazingira halisi ya jamii. Utafiti ulifanywa kwa kutumia mbinu ya kiethonografia iliyohusisha kushiriki, kushuhudia na kuhoji pamoja na udurusu wa nyaraka zilitumika katika kukusanya nyimbo na vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi katika kila tapo au kipindi. Nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma na ile ya Wigo au Uigaji (Ethnopoetics and Emic Theory) ndizo zilizotumika katika kufanikisha utafiti huu. Uchanganuzi wa data na matokeo ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Makala hii imedhihirisha kuwa matapo yaliyopo katika fasihi andishi; Usasa na Usasaleo, ndiyo hujulikana kama Ukale na Ujadi katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Aidha, makala imependekeza kufanyika kwa tafiti nyingine mbalimbali katika fasihi simulizi.

**APA CITATION**

Lukamika, K. M. (2022). Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 58-68. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948.

**CHICAGO CITATION**

Lukamika, Kibigo Mary. 2022. “Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?”. *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 58-68. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948.

**HARVARD CITATION**

Lukamika, K. M. (2022) “Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?”, *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 58-68. doi: 10.37284/jammk.5.2.948.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**IEEE CITATION**
K. M. Lukamika, "Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 58-68, Nov. 2022.

**MLA CITATION**
Lukamika, Kibigo Mary. "Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi?". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Nov. 2022, pp. 58-68, doi:10.37284/jammk.5.2.948.

## UTANGULIZI

Dhana hii ya 'Fasihi Simulizi' imezua utata miongoni mwa watafiti, hususani katika uchaguzi wa istilahi sahihi ya kuirejelea kutoka tafiti tafsiri ya Kiingereza '*Oral Literature*.' Tukirejelea jamii zenye hadhi tunaona kwamba neno '*literature*' lina misingi yake katika maandishi wakati Waasia, Waafrika na Waingereza walipokuwa hawajui kuandika. Finnegan (1970, 1992 & 2012), anasema kuwa fasihi simulizi yaweza kuelezwa kutegemea msanii ambaye huiumba kwa maneno katika tukio. Kama anavyosema Wanjala (2011), maandishi na fasihi ni vitu viwili tofauti, anaeleza kuwa hii ndiyo sababu wasanii au watafiti wengi wametumia istilahi tofauti kuirejelea fasihi isiyoandikwa; *Oral Literature, Past or Unwritten Literature, Popular or Traditional Literature, Folk Art, Forklore, Verbal Art, Primitive Art Forms or Orature.* Mtaalamu huyu anafafanua zaidi kwa kusema kuwa tukihusisha fasihi (*literature*) na maandishi ni sawa na kusema jamii zisizotumia hati hazina fasihi. Kulingana na maoni yetu, fasihi simulizi ni aina ya sanaa inayowasilishwa kwa ubunifu kupitia lugha ambayo inahifadhiwa kichwani. Hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo. Ingawa Finnegan (1971) anadai kuwa Waafrika hawakuwa na fasihi, madai haya yanakinzana na utafiti huu kwa kwani, Waswahili katika muktadha wa makala hii wameonesha kuwa walikuwa na fasihi. Kwa hivyo, matapo katika fasihi simulizi ya Kiswahili si dhana ngeni. Hali hii ni muhimu kwa vile fasihi simulizi huwasilishwa na fanani au mtambaji, huwa na hadhira tendi, jukwaa na mada inayowasilishwa. Hali hii ndiyo hutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi.

Mawazo yetu na ya wataalam kama vile Msokile (1992) na ya Wanjala (2011) yanawiana kwa vile yanaeleza kuwa fasihi simulizi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha. Kazi hii huhifadhiwa kichwani na kusambazwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo, mwasilishaji mkuu akiwa ni fanani. Hivyo, fasihi simulizi imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi hadi kizazi. Njogu na wenzake (2006) nao wanaeleza kuwa fasihi simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema ya kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Mrikaria (2007) anasema kuwa fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali. Anadai kuwa ilianza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha kama chombo cha mawasiliano. Hapo ndipo binadamu alipoanza kuimba, kutumia methali, vitendawili, hadithi na kadhalika. Hivyo, fasihi simulizi kimsingi imejengwa katika mfumo uliozoeleka wa kufikisha ujumbe kwa hadhira na ulilenga zaidi katika kurithisha mila, desturi na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa nyimbo, hadithi, mashairi, na hata michezo ya ujasiri na majigambo. Anaongezea kuwa, awali fasihi simulizi ilihifadhiwa kichwani lakini ilibadilishwa na ikaanza kuhifadhiwa kimaandishi. Ntarangwi (2004), anasema kwamba kazi nyingi za fasihi simulizi hapo awali zilikuwa katika masimulizi lakini sasa zimehifadhiwa katika maandishi na huratibiwa kama kazi za fasihi.

Balisdya (1991) akikubaliana na mawazo ya Okpewho (1979) anasema kuwa fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumizi wake. Aidha, sanaa hii hutumia maneno kutoa dhana fulani na kuenezwa kwake hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binadamu katika kujieleza.

Fasili zote zinazungumzia kitu kilekile; kwamba fasihi simulizi inategemea sana kuwapo kwa fanani, hadhira, jukwaa na mada inayotendwa. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa fasihi simulizi ni sanaa inayotumia lugha ya kisanaa ili kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa kwa njia ya mdomo au masimulizi. Hata hivyo, historia hujirudia. Kwa mfano, mapenzi, siasa, unyonge wa wanawake, ukombozi, uchawi na ushirikina, uzazi, ndoa na migogoro ya kitabaka. Isitoshe, fasili za wataalamu hawa zinatuelekeza kutoa kauli kuwa, fasihi simulizi ndiyo mama mzazi wa fasihi andishi,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

kwa vile ni ya awali na ikahifadhiwa tu kimaandishi kama anavyohitimisha Wanjala (2011) katika kitabu chake cha *Kitovu cha Fasihi Simulizi*.

Kwa mujibu wa Wanjala (2011), wataalamu wengi wamekuwa wakiongozwa na nadharia za jadi kutoa fasili na sifa za fasihi simulizi. Hata hivyo, maendeleo na mabadiliko yanayojiri katika jamii kila uchao yamemwezesha mtaalamu huyu kuibuka na maoni tofauti na kuweza kubadilisha mtazamo huu kama inavyodhihirika katika baadhi ya maelezo yake. Kwa mfano, hivi sasa, fasihi simulizi inawasilishwa kupitia kwa runinga au rungoya. Fasihi simulizi yaweza kuhifadhiwa kandani, kwenye santuri, diski tepetevu na katika tarakilishi. Anatoa mfano wa fasihi simulizi kutoweza kuwa na wakati na muktadha maalumu, pale anapoeleza kuwa nyiso za Wabukusu sasa haziimbwi tu katika muktadha wa tohara bali huimbwa katika muktadha wa arusi na matanga.

Jambo muhimu linalojitokeza hapa ni kwamba, tija kuu ya Sayansi na Teknolojia kwa fasihi simulizi ni kuvumbua mbinu mwafaka za kuhifadhi na kuieneza fasihi simulizi. Hata hivyo, Wanjala (2011) anadai kuwa mbinu hizi za kuhifadhi na kuieneza fasihi simulizi hupuuza umuhimu wa utendaji na kwa hivyo huondoa ule utamu wa fasihi simulizi. Anaonesha namna uhifadhi wa fasihi simulizi kwenye maandishi ulivyo mzunguko unaoturudisha kule kule tulikotoka kwa Ukale na Ujadi. Kwa hivyo, watu wengi wametambua kuwa fasihi simulizi ndiyo fasihi ya awali. Ndiyo maana leo, riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi yanaigizwa kwenye jukwaa, rungoya, wavuti au runinga ili kuyatilia uhalisi na uhai kupitia utendaji. Matei (2011) anaeleza kuwa ingawa kumekuwa na mabadiliko mengi katika fasihi simulizi, ni muhimu kujikita katika vipengele vyake kama vile, fanani au msanii, hadhira, kipera cha fasihi simulizi, mandhari au mazingira, lugha na shughuli ya kijamii ambamo utungo huibuka.

M'ngaruthi (2008) anaunga mkono mawazo hayana kuonyesha kuwa, hakika kuna ufaraguzi ambao umeibuka katika fasihi simulizi. Hali hii huweza kujitokeza katika miktadha mbalimbali. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali halisi niliyoijadili hapo juu. Wimbo ufuatao wa Bahati unatupa kigezo namna ambavyo fasihi simulizi inaweza kuonesha hali halisi ya hisia za binadamu. Mfano huu unaweza kulinganishwa na mapenzi ya Mungu Mwenyezi kwa binadamu wake, hali inayodhihirisha matumizi ya nadharia ya wigo:

Unapotaka kumweleza mchumba wako namna unavyompenda, ili akuelewe vizuri zaidi, utampigia simu badala ya kumwandikia barua. Aidha, unapomwimbia wimbo wa mapenzi kama vile taarab au wimbo wowote wa mahaba kwa mfano wimbo wa Kelvin Kioko Bahati (2014) kuhusu:

> *Ni barua ngapi nimeandika kwa njia ya muziki?*
>
> *Na nyimbo ngapi nimeandika zisizo za riziki* × *2*
>
> *Nikikuita mpenzi, mpenzi, mpenzi, nikikuita dadi* × *4*

Basi, katika hali hii mpenzi wako huweza kukuelewa vyema zaidi na kupata zile hisi za ndani zinazotoa udhati wa mahaba. Ingawa hivyo, wimbo huu uliimbwa na Bahati akiwa na dhamira ya kumsifu Mwenyezi Mungu. Hali hii inadhihirika wazi anapomuita Mungu 'dadi' kuashiria baba.

## KIUNZI CHA NADHARIA

Makala hii imejikita katika kiunzi cha Nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma na ya Wigo au Uigaji. Kwa mujibu wa Foley (1995), Nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma ilianzishwa kule Marekani miaka ya 1950-1960 na waasisi wake walikuwa Dennis Tedlock na Dell Hymes. Waliibuni kutokana na utafiti wao wa matini simulizi miongoni mwa Wamarekani. Nadharia hii iliwahi kutumiwa na wataalam kama vile Wanjala (2015). Kimsingi, Nadharia hii inajihusisha na upangaji wa matini simulizi kishairi kwa misingi ya taaluma za Isimu-Amali, Isimu-Jamii, Ethnografia ya Mawasiliano na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ndani ya Muktadha wa Utendaji. Dennis anasisitiza kuwa usimulizi katika matini unafaa kupangwa kwa njia ya mistari kama ilivyotolewa na fanani katika utendaji wa fani ya usemaji. Uwasilishaji huu hutumia vipengele kama vile, uradidi, shadda, kiimbo na matumizi ya jazanda. Anasisitiza kuwa utafiti wa nyanjani ni lazima. Harvilahti (2001) anachangia nadharia hii kwa kusema kuwa, maana katika matini simulizi huumbwa na vipande sauti pamoja na utamaduni wa jamii husika. Nadharia ya wigo au Uigaji kwa upande mwingine iliasisiwa na akina Plato na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

Aristotle. Nadharia hii inasisitiza kuwa binadamu alianza kuwa mbunifu kwa kuiga maumbile na ulimwengu unaomzunguka. Plato anahusisha wigo na dhana ya Uungu na kueleza kuwa maumbile tuyaonayo duniani ni uigaji wa maumbile halisi ya mbinguni. Katika muktadha huu, nadharia hizi ni faafu kwa utafiti huu kwa vile utafiti wetu ulijikita katika fasihi simulizi na upangaji wa mistari na fanani husika. Aidha, wigo ni dhana ambayo imejitokeza katika kazi hii hususan tunapoona namna fanani anaiga hisia za Mungu katika nyimbo zilizotumiwa.

## MATAPO KATIKA FASIHI SIMULIZI

Kimsingi, matapo katika fasihi simulizi hujitokeza katika awamu nne: Urasimi; Urasimi Mkongwe (850 – 325 KYM) na Urasimi Mpya (1680 – 1780 BYM), Ulimbwende (1790 – 1870 BYM), Uhalisia (1914 - 1945) na Usasa na Usasaleo (1945 – hadi waleo /Ukale) na Ujadi (wakati fasihi simulizi ilivyoanza).

Aghalabu, matapo hudhihirika katika fasihi andishi. Ingawa kuna matapo mengi ya fasihi simulizi ambayo yamejitokeza ulimwenguni kufikia sasa, kuna yale ambayo yameshughulikiwa zaidi katika tahakiki na nadharia za sanaa. Matapo ni vipindi bainifu vya kihistoria vinavyoonyesha maendeleo na mabadiliko katika fasihi. Sifa zake huwa teule na ambazo huelekeza utungaji wa kazi za fasihi. Hivyo, fanani hana budi kuzibainisha wazi sifa za kila tapo ili aweze kutunga kazi kulingana na kanuni hizo. Kwa hivyo, kila tapo hutegemea mtunzi wa kazi husika ya fasihi. Kwa upande mwingine, nadharia ni mwongozo unaomwelekeza mpokezi wa kazi ya fasihi kuifahamu kwa undani zaidi. Kulingana na Wanjala (2011), nadharia inaweza kuundwa kutokana na tajriba ya mtu binafsi au juhudi za kikundi cha watu. Hivyo basi, nadharia huwasaidia wapokezi wa kazi za kifasihi katika juhudi za kuutathmini ufanisi wa fanani. Nadharia huwa kama mkongojo wa anayeipokea kazi ya fasihi kwa vile huweka wazi vigezo na taratibu za kuzingatiwa ili uhakiki uwe thabiti na wa kuaminiwa. Ni kama dira inayowapa wapokezi wa kazi za kifasihi vigezo sawa vya kuzitathmini kazi za fasihi.

Katika msingi huu, tapo na nadharia si sawa. Katika msingi huu, matapo ni vipindi na ndanimwe tunaweza kupata nadharia anuwai. Wanjala (2020) akiunga mkono mawazo ya Okpewho (1979), anatoa taswira mathalan katika kipindi cha Usasa na Usasaleo, kuna nadharia kama vile ya Mwingilianomatini na Usemezano. Kwa upande mwingine, nadharia haiwezi kubeba matapo au tapo ndanimwe. Wanjala (keshatajwa) anatupatia taswira ya nadharia na tapo kwa kufananisha na mti na matawi yake. Anasema kwamba, nadharia haiwezi kubeba matapo ndani mwake. Hii ina maana kuwa tapo kama kipindi ni mfano wa mti ambao unaweza kuwa na matawi mengi ambayo ni kama nadharia.

Vinginevyo, haiwezekani tawi moja kubeba mti au miti mingi.

Matapo teule katika Fasihi Simulizi ni manne. Nayo ni:

- Urasimi i) Urasimi Mkongwe (850 – 325 KYM); ii) Urasimi Mpya (1680 – 1780 BYM)
- Ulimbwende (1790 – 1870 baada ya karne ya 18)
- Uhalisia (kuanzia nyakati za Malkia Victoria na wakati wa Mapinduzi ya Viwanda, 1914-1918).
- Usasa na Usasaleo (1945 hadi leo) / Ukale na Ukalejadi – wakati wa hapo awali zaidi fasihi simulizi ilipoibuka na binadamu kuanza kutumia lugha.

### Kipindi cha Urasimi

Kwa vile tapo ni kipindi bainifu cha kihistoria, tunaona kuwa mwanzoni kulikuwa na kipindi cha Urasimi Mkongwe kisha kukawa na kile cha Urasimi Mpya. Kimsingi, Wayunani na Wagiriki wa jadi waliweka misingi mbalimbali katika taaluma nyingi duniani. Mawazo mengi ya wanataaluma hao yalinakiliwa na kwa hivyo tunaporejelea nadharia ya uhakiki, huwa tunaanza nao. Urasimi ni kipindi maalumu ambapo misingi ya kazi za sanaa huwekwa na kukubalika na jamii kuwa mfano na kipimo bora cha sanaa. Wanafalsafa hao ambao ni Socrates, Plato na Aristotle waliona fasihi kama zao la msukumo wa kiungu katika kuumba. Tapo la Urasimi lilitokea na kujikita katika sehemu mbili ambazo zilikuwa ni Urasimi Mkongwe na Urasimi Mpya. Waasisi wa Urasimi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

Mkongwe ni Wayunani au Wagiriki wa kale ambao waliweka misingi mbalimbali katika taaluma nyingi duniani. Urasimi Mkongwe uliasisiwa mnamo mwaka wa 850 – 325 Kabla ya Masihi. Waasisi wa tapo hili ni Socrates, Plato na Aristotle. Kwa mfano Aristotle aliamini kuwa fasihi ina umuhimu zaidi ya kuiga kikasuku. Aidha, pamoja na mawazo mengine, alidai kuwa fasihi inaweza kuwa na ujumbe muhimu kwa binadamu wote wakati wowote ule. Kulingana na Warasimi, uandishi bora ni ule ulio na sifa zifuatazo:

- Matumizi ya semi na methali zinazoafikiana na maudhui yanayowasilishwa.
- Matumizi ya lugha inayooana na muktadha unaoizalisha.
- Uwezo wa kutumia lugha tukufu au lugha teule.
- Uwezo wa kuyahusisha mambo yaliyosemwa na mazingira yote yanayoizalisha hali hiyo. Mazingira hayo kwa vyovyote vile hutuangazia maudhui muhimu yanayoelezwa. Katika hali hii, kuna nyimbo za Zaburi zilizotungwa na Daudi katika Bibilia. Nyimbo hizi zilitungwa Kabla ya Masihi. Kwa mfano, Zaburi 23: 1 – 16. Wimbo huu unaimbwa hivi:

  *Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu.*

  *Katika malisho ya majani mabichi hunilaza,*

  *Kando ya maji ya utulivu huniongoza.*

  *Katika njia za haki kwa ajili ya jina lake*

  *Nami nitakaa nyumbani mwa BWANA, siku zote za maisha yangu ×2*

Plato anaeleza kuwa ushairi ueleze mambo mazuri pekee ya ushujaa na utawala wa wananchi. Anaongezea kuwa ushairi uzungumzie dini, muziki na matendo ya kishujaa ya nchi, ushairi umtumikie mtu, umtakase roho, umfanye kutii sheria na kumfanya awe mzalendo. Baadhi ya nyimbo za Daudi bin Jesse katika Biblia kama *Zaburi* 100 zinajitokeza katika tapo hili la fasihi simulizi.

Aidha, kuliibuka Urasimi Mpya ambao ni wakati ambapo kulikuwa na hali ya kurejeshwa tena kwa kanuni za utunzi wa sanaa zilizoheshimiwa sana na Warasimi. Mtazamo huu hata hivyo, haukufuata mkondo wa moja kwa moja wa Urasimi Mkongwe. Kipindi hiki kilishamiri zaidi katika karne ya 18. Falsafa ya wakati huo ilikuwa ya kisayansi. Waandishi na wahakiki mashuhuri wa wakati huo walikuwa: Ben Johnson, Alexander Pope na Jonathan Swift. Warasimi Wapya waliiga mitindo mingi ya Warasimi Wakongwe kama vile, kuziamini kaida fulani za kuongoza utunzi na kuwasilisha fasihi. Kwa upande wa Kiswahili, kuna kitabu cha Amri Abed chenye mada *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Mwandishi huyu aliorodhesha kanuni za kutunga mashairi. Mfano mzuri wa utanzu unaoingia katika tapo hili ni nyimbo za taarab; mojawapo ya kitanzu cha fasihi simulizi kinachotoka ndani ya kitanzu cha ushairi simulizi ambamo tunapata kitanzu cha nyimbo.

Ushairi ni utanzu unaotumia lugha ya mkato kufikisha ujumbe wake kwa jamii (Kahigi na Mulokozi,1973). Nyimbo za taarab, ndani ya Visiwa vya Zanzibar zina historia ndefu. Historia hiyo ilianza miaka ya 1870 (kipindi cha Urasimi Mpya) – wakati wa utawala wa Sultani Seyyid Barghash. Wakati huo, taarab iliingizwa Zanzibar kama nyimbo za kumbi za utawala na ziliimbwa kwa lugha ya Kiarabu. Ntarangwi (2004), anaeleza kuwa vina na silabi ziliingizwa katika ushairi kutokana na athari za Uarabu. Kulingana na maoni ya wataalamu wengi, taarab ziliwatumbuiza viongozi wenye asili ya Kiarabu, wafanyabiashara na wananchi wote wa kawaida. Ziliendelea kutumia lugha ya Kiarabu hadi kufikia enzi ya utawala wa Sultan Barghash ambapo lugha ya Kiswahili ilianza kutumika. Katika hali hii, lugha tukufu au teule ilitumiwa kama Warasimi wanavyopendekeza.

Hata hivyo, mabadiliko hayo yalihusishwa na mwimbaji wa taarab aliyesifiwa sana Zanzibar na nchi za nje, Siti binti Saad (mwimbaji wa mwanzo kabisa wa kike).

Taarab ya Siti binti Saad inafaa katika kipindi hiki cha Urasimi Mpya kwa vile ilikuwa na uwezo wa kuyahusisha mambo yaliyosemwa na mazingira. Aidha, hutuangazia maudhui muhimu yaliyoelezwa, kwa mfano katika kipindi hicho ambapo matajiri walikuwa wakiwaonea sana maskini na walipofikishwa mbele ya hakimu walitoa hongo na kuachwa huru. Washtaki wenye haki ndio waliofungwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

Kama tujuavyo, ushairi wa kirasimi wa Kiswahili ulisisitiza umuhimu wa kuwa na vina na mizani katika shairi. Hali inayojitokeza katika utunzi wa Siti binti Saad wa *Kijiti*, ndio uliompa sifa kubwa, ukielezea kisa cha kweli kilichomkuta mwanamke mmoja kutoka mwambao wa Tanganyika:

**Kijiti**

*Tazameni tazameni, aliyofanya kijiti*

*Kumchukua mgeni, kumchezesha foliti*

*Kendanae maguguni, kamrejesha maiti*

*Tuliondoka nyumbani, hakutuaga ruhusa*

*Na tende yetu kapuni, amenichukua kabisa*

*Magoma yako Chukwani, mauti Sharifmsa*

*Kijiti alinambia, ondoka mama twenende*

*Laiti ningelijua, ningekataa nisende*

*Kijiti unaniuwa, kwa pegi moja ya tende*

Mwanamke huyo alipofika alikutana na tajiri mmoja, aliyejifanya anampenda, akamchukua na kukaa naye, akastarehe naye, kisha akamwua. Tajiri huyo alishtakiwa, walikuwapo mashahidi wawili walioshuhudia tukio hilo lakini kwa vile alikuwa tajiri/mkwasi, alitoa pesa na kesi ikawageukia wale mashahidi na kufungwa. Mfano huu unakidhi matakwa ya kuwekwa kwa kipindi hiki cha urasimi kwa ajili ya mambo ya kuwako kwa vina na mizani.

**Tapo la Ulimbwende**

Ulimbwende ni neno linalotokana na neno la Kiingereza '*Romance*' lililokuwa na maana ya mchanganyiko wa lugha ya Kilatini na lahaja za Tutonic – dhana inayoashiria hisi za mapenzi. Hata hivyo, neno hili lilibadilika na kuwa mwamko wa kihistoria na kimatini katika karne ya 18. Ni pingamizi dhidi ya kaida za sanaa zilizowekwa na Warasimi. Ulimbwende ulitokana na urasimi mpya. Tapo hili humtazama binadamu kama kitovu ama chimbuko la sanaa. Walimbwende walisisitiza uhuru wa mtu binafsi. Kimsingi, ulikuwa mwamko wa kitaaluma uliochipuka mnamo karne ya 19 na ambao uliandamana na matumaini ya fanaka katika ngazi mbalimbali za maisha ya binadamu. Ni mtazamo uliotia fora kati ya mwaka wa 1790 na 1870. Ingawa mtazamo huu wa fasihi ulisambaa sehemu mbalimbali za Uropa katika miaka tofautitofauti, Waingereza wawili ndio waliosababisha usambazaji wake kama mkabala wa kitaaluma wa kuishughulikia fasihi. Nao ni William Wordsworth na Samuel T. Coleridge. Majira ya ulimbwende yalikuwa ya kimapinduzi. Katika mwaka wa 1789, mapinduzi ya kisiasa yalizuka huko Ufaransa. Sehemu nyingine za Uropa zilitetemeshwa na matokeo ya mapinduzi haya. Hali hiyo ilikuwa kinyume na muktadha uliopalilia, kukuza na kuimarisha Urasimi Mpya. William Wordsworth alikuwa mtetezi wa demokrasia na alisisitiza uhuru wa mtu binafsi dhidi ya mikatale ya utumwa iliyopachikwa na wanajamii wengine. Hiyo ndiyo sababu inayomfanya Wordsworth kuweza kutunga mashairi yanayosisitiza usawa wa wanadamu wote (*equality of all human beings*). Kwa mfano, alitunga mashairi kama vile; '*A Female Vigrant*' ambayo yanawashambulia matajiri, walafi, vita na dhuluma zinazoletwa na ukandamizaji wa wanajamii na wanajamii wengine.

Wordsworth aliathiriwa pakubwa na mwanafalsafa Hartley. Hartley aliamini kuwa uumbaji wa dhana hutegemea hisi za muumbaji huyo. Kulingana na Hartley, ubongo wa mtu hauumbi wala kuibusha ujuzi wa aina yoyote. Kinyume chake, hisi ndizo huzalisha utaalamu wa aina yoyote. Hata maadili vilevile hutokana na hisi. Hivyo basi, walimbwende waliweza kuathiriwa na mawazo haya ya Hartley. Katika tungo zao, waliziachilia hisi kuutawala urazini wao. Hatimaye, hisi hizo zilizipa miundo dhana walizotaka kuziwasilisha. Ulimbwende wa Kimagharibi ulikuwa zao la kihistoria kwa kuwa kwa kiasi kikubwa ulipingana moja kwa moja na Urasimi Mpya wa Kimagharibi. Kama tulivyotaja, Urasimi Mpya ulifuata kanuni katika utunzi na uhakiki wa kazi za fasihi. Mwishowe, Urasimi Mpya ulizingatia zaidi kanuni za utunzi kuliko ubunifu wa utunzi. Jambo hili liliwafungia nje watunzi waliotaka kufuata silika zao. Mielekeo ya tapo la Ulimbwende ilipoanza kupata waitifaki wengi, watunzi wa aina hii waliwaunga mkono. Ulimbwende huchukulia fasihi kama zao la mtu binafsi. Hivyo basi, unasisitiza ubunifu wa msanii katika kuandika au kuiwasilisha kazi ya sanaa. Kwa hivyo, Ulimbwende ulijikita katika sifa zifuatazo:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

**Sifa za Ulimbwende**

- **Ndoto au njozi:** Walimbwende waliamini kuachilia ubongo ili akili iamke. Walichukulia ulazaji ubongo kama njia ya kuamsha akili.

- **Mawazo na matokeo ya ajabu**: Hadithi za walimbwende zilianza na viumbe vya ajabu kama vile zimwi au jitu.

- Walijishughulisha na mambo huru na kuzingatia aina zote za utunzi kama vile hekaya na hadithi za majitu, vita na wanyama wakali. Kimsingi, hadithi hizi zote ziliyazingira maisha ya binadamu.

- Mawazo ya walimbwende yanatokana na binadamu wote wa kawaida katika tamaduni za kale au pande za dunia ambazo hazijachafuliwa na usasa. Walimtazama binadamu katika uasili wake.

- Ulimbwende ulianza mahali pa kawaida na kukiuka mipaka katika uwanja wa uhalisia. Ulianza katika hali ya kutunga kuhusu mambo ya asili kama vile misitu, mabonde na miamba.

- Mianzo ya kazi za fasihi ya kipindi hiki ni ya ajabu kama vile wito wa ajabu, mtazamo wa kwanza wa kimapenzi, safari ya pweke, kupitia nchi za kutisha, vita na viumbe wa kutisha.

- Washairi wake wakuu walikuwa kama vile: William Wordsworth, John Keats, Coleridge, Von Schegel na William Blake ambao maoni yao yalikuwa kuunganisha dunia dhahania na dunia halisi. Hawa, wanauona ushairi kama picha ya mtu na maumbile ya ulimwengu wake.

- Kulingana na Wordsworth, utunzi una chanzo chake katika jazba. Kwa hivyo, mwandishi aamshe hisia za msomaji. Mshairi atumie lugha ya anaowaandikia. Utulivu wa ubongo humpumbaza mshairi na kumweka katika ulimwengu wa ndoto na upekee huku akiongea na maumbile.

- Wordsworth anasisitiza kuwa maumbile ndiyo mlezi, kiongozi na muuguzi wa maisha. Kwa hivyo, kazi ya fasihi izungumzie maumbile na mazingira ya binadamu.

Sifa hizi zinatuelekeza kutambua kuwa Ulimbwende wa Kiswahili ulikuwa tofauti na ule wa Ulaya. Kwa mfano, tukiangazia ushairi andishi wa Kiswahili, walimbwende walizua ushairi huru usio na vina wala mizani, wao walijikita katika maudhui tu. Katika kipindi hiki pia washairi kama Lord Byron na Bums walisisitiza haki za kibinadamu, hali ambayo inadaiwa haikuwepo awali. Kwa upande mwingine, katika Fasihi Simulizi, kuliibuka nyimbo nyingi zilizosheheni sifa hizi za ulimbwende. Walitumia fantasia (ndoto) kueleza masuala ya kijamii. Hatua hii ilichukua mkondo mpya uliokinzana na tapo la Urasimi ambalo aghalabu liliziona sifa za vina na mizani kuwa ni roho ya ushairi. Tapo hili linasisitiza ubunifu na hisia. Kirumbi (1975) naye anaamini kwamba chanzo cha fasihi ni “Hisi” (Hisia) za mtu au wengi katika jamii. Hisi hizi huibuka katika mazingira mbalimbali kama vile sherehe za harusi, matanga na kilimo miongoni mwa mengine. Isitoshe, wanadai kuwa fasihi huweza kuelezea mapenzi lakini fasihi yenyewe si mapenzi. Tazama mfano ufuatao:

**Hisi ya Furaha**

Mfano wa kwanza wa shairi simulizi lililoshamiri katika tapo la Ulimbwende ni la **Cheka kwa furaha**

*Dhiki ni kama mzaha, asiyecheka nani?*

*Haya cheka kha kha kha, ndiyo ada ya dunia.*

*Basi cheka kwa! kwa! kwa! Usafike moyo wako.*

Ndiposa Kahigi na Mulokozi (1979) wanasema kuwa ushairi ni lazima uguse hisi, lazima umsisimue anayeusema, kuusoma na kuuimba na yule ausikilizae. Wanaongezea kuwa shairi lisilogusa hisi ni kavu na butu, hata kama limesarifiwa katika vina na urari wa mizani, shairi hilo litaishia katika kuhubiri tu.

**Tapo la Uhalisia**

Tapo hili la fasihi pia huitwa Uyakinifu. Liliibuka mnamo 1914-1918. Hata hivyo, wataalamu wengine wanaeleza kuwa tapo hili liliwahi kutokea katika karne ya 19 na 20 na hata pengine litaendelea kutuathiri katika karne hii ya 21. Tapo hili liliwekewa msingi na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel katika kitabu chake kinachojulikana

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

kama *Aesthetik* (Ujumi). Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo. Ni mojawapo ya matapo maarufu katika ulimwengu wa fasihi na lenye athari kubwa sana. Chini ya tapo hili, nadharia zilizozuliwa ni kama vile; Uhalisiajabu, Uhalisia wa Kijamaa, Uhalisia wa Kihakiki miongoni mwa nyingine. Uhalisia huhitaji msanii kutupilia mambo ya kubuni na badala yake kuwaza. 'Uhalisia' kama dhana, hutumiwa kwa maana mbili kuu. Kwanza, kuelezea tapo la kipindi maalum cha kihistoria katika fasihi za Ulaya. Pili, kuelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambako kazi za kifasihi zinachukuliwa kama zinazohifadhi au kuakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi. Waasisi wa tapo hili, hawatilii maanani maandishi, bali mambo yaliyo dhahiri au wazi katika sanaa. Wanauhalisia wanasisitiza zaidi ukweli wa mambo kwa mujibu wa muktadha, historia na jamii husika. Hata hivyo, tapo hili huvuka mipaka ya kihistoria. Kwa kiasi kikubwa, kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia, zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika (Wamitila, 2006). Kulingana na wanatapo hili, hadhira ni dhana muhimu sana. Waasisi wakuu wa tapo hili ni pamoja na Defoe, Richardson, Fielding, Dickens na Balzac. Hawa wanaeleza kuwa, ili fasihi iwe na manufaa katika jamii, inafaa kuwa chombo cha kuichambua, kuikosoa, kuishauri na kuiokoa jamii. Dhana ya fasihi kuwa kioo cha jamii ilitokana na tapo la Uhalisia.

***Sifa za Tapo la Uhalisia***

- Kuzingatia kwa hali ya juu uhalisia katika kuwakilisha maisha kupitia sanaa ya fasihi.
- Kuonesha mkabala wa wasomi, waandishi wa fasihi, falsafa na siasa.
- Sifa ya mtunzi wa fasihi au sanaa.
- Kiwango cha mtunzi kuwasilisha maisha jinsi yalivyo kwa uhuru au demokrasia.

Wimbo ufuatao unaakisi sifa za tapo hili kwa vile ulitungwa na kuimbwa katika kipindi hicho:

Wimbo wa Mbaraka Mwinshehe akiwa na kundi la Morogoro Jazz Band, ulioshamiri enzi za miaka ya 90 wenye mada :

***Utanikondesha Maria***

*Fanani: Ooooh Maria,*

*Wote: Ooooh kweli unanitupa,*

*Fanani: Mimi sikutegemea kamaa*

*Wote: Siku moja utakuja sema,*

*Fanani: Mimi nilivyoamini*

*Wote: tutaishi milele*

*Fanani: Ooooh Maria,*

*Wote: Ooooh wanipa machungu,*

*Fanani: Mimi nitabaki*

*Wote: peke yangu,*

*Fanani: Hapo ndipo wazo litazidi, Wote: Sitarudi nyuma.*

*Fanani: Ooooh Maria,*

*Wote: Ooooh unanipa machungu,*

*Fanani: Mawazo yote yatanizidi*

*Wote: Najua utaondokaa mamaa,*

*Fanani: Kwa ajili ya mazoea, Wote: nitakonda.*

Ndiposa Wamitila (2003) anatueleza kuwa, takriban shughuli zote za binadamu kama kulima, kusuka, kutahiri, kuoa, kulea, kufariji, kuliwaza, kutaliki na kuzika huandamana na uimbaji. Aidha, asili ya ushairi ni wimbo.

**Tapo la Usasa na Usasaleo / Ukale na Ukalejadi**

Tapo hili liliibuka mnamo mwaka wa 1945 hadi sasa. Katika tapo hili tunapata nadharia kama vile:

Mwingilianomatini, Usemezano na Ukanivali miongoni mwa nyingine. Dhana hizi mbili yaani Usasa na Usasaleo hutumiwa kuelezea mielekeo ya kitamaduni na kisanaa inayohusishwa kwa kiasi kikubwa na karne ya 20. Tatizo kubwa kuzihusu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

dhana hizi ni kuiweka mipaka wazi kati yake. Wamitila (2003) anaeleza kuwa, aghalabu kile ambacho mhakiki mmoja atakieleza kama Usasa, mwenzake atakiona kama Usasaleo. Kimsingi, Abrams (1993) anadai kuwa dhana ya Usasa hutumiwa kuelezea au kuzitambulisha sifa mpya za dhamira, tanzu, dhana na mitindo ya kifasihi inayohusishwa na miongo ya kwanza ya karne ya ishirini. Wakati unaohusishwa sana na tapo hili ni baada ya Vita Vikuu vya Pili. Waasisi wa tapo hili, ni wanafalsafa walioishia kudadisi misingi ya miundo ya kijamii, kidini, kimaadili na mitazamo ya kijadi kumhusu binadamu kama kiumbe. Hivyo basi, suala la wakati wa kuzuka au kuchipuka kwa Usasa na Usasaleo ni la kimjadala au hata kwa kiasi kikubwa la kubahatisha. Kwa upande mwingine, dhana za Ukale na Ukalejadi ni kama upande mwingine wa sarafu ya Usasa na Usasaleo kwa vile, kile kinachoitwa Usasa katika fasihi andishi, katika fasihi simulizi ni Ukale na Ukalejadi.

***Sifa za Usasa na Usasaleo / Ukale na Ukalejadi***

- Mwingilianomatini; kwa mfano, mgombeaji wa kiti cha Urais kwa tiketi ya NASA Mheshimiwa Raila Amollo Odinga aliposema yeye ndiye Joshua wa kuwasaidia Wakenya kuvuka Mto Misri na kuwapeleka hadi Kanaani, hali au muktadha huu unatuelekeza kutambua kuwa ili uweze kuelewa usemi huu, ni sharti uyahusishe na matini ya Biblia. Katika Ukale na Ukalejadi, hali hii hujitokeza katika mwingilianotanzu.
- Kuchanganya ndimi; lugha mbili au zaidi huweza kuchanganywa ili fanani aweze kueleweka barabara.
- Ujarabati; hali hii hujitokeza katika Usasa na Usasaleo. Kwa mfano, nyimbo za kisasa zinapokiuka itikadi na utamaduni. Kwa mfano nyiso zinapoimbwa katika sherehe za arusi.
- Ubunifu wa kiwango cha juu na kukiuka Ukale. Kwa mfano, matumizi ya Teknolojia katika uwasilishaji wa maumbo ya fasihi simulizi kupitia 'Facebook,' 'Twitter,' 'Instagram' na vikundi vya 'Whatsapp' na kadhalika.
- Uvumbuzi wa mitindo mipya ya nyimbo.
- Ubinafsi; kwa vile jamii haifai kuihukumu kazi ya msanii.
- Usomi; kwa vile wanaongozwa na hekima katika kufaragua mitindo mipya na hata kurejelea historia, kwa mujibu wa wasanii wa fasihi simulizi.

***Mfano wa wimbo katika tapo hili ni:***

Shairi la Mapenzi lililotungwa na Idd Ninga; Septemba 10, 2014

*1. Wewe ndie 'star' yangu, usiku wamulikia,*

*Uniachi peke yangu, ukaniacha ninalia,*

*Nikabaki peke yangu, mbali ukanikimbia,*

*Nakupenda ewe wangu, kwengine siwezi kwenda.*

*2. Wewe ndie 'moon' yangu, usiku waangazia,*

*Ewe ndie 'lamp' yangu, mwanga wanimulikia,*

*Nakuhitaji ewe wangu, la sivyo nitapofuka,*

*Nakupenda ewe wangu, kwengine siwezi kwenda.*

*3. Wewe ni 'honey' yangu, nyuki sitowafukuza,*

*Kuvunja mzinga wangu, ni jambo nisiloweza,*

*Nikabaki peke yangu, ulimwengu kuniweza,*

*Nakupenda ewe wangu, kwengine siwezi kwenda.*

*4. Ewe ndio 'sheet'yangu, yanilinda kwa baridi,*

*Wewe ndie 'coat' yangu, daima sitokaidi,*

*Takulinda vazi langu, ili nije kufaidi,*

*Nakupenda ewe wangu, kwengine siwezi kwenda.*

Wimbo huu unaafiki kuwekwa katika tapo hili la Usasa na Usasaleo kwa vile umesheheni baadhi ya sifa za tapo hili kama vile kuchanganya ndimi, kwa mfano neno kama vile; '*honey*' kurejelea mpenziwe alivyo mtamu kama asali. Aidha, kuna vipengele vya usomi, ubinafsi, mwingilianomatini, na hata chembechembe za utupiliaji mbali wa ukale. Hata

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

hivyo, ni muhimu kutaja kuwa chochote kile kinachoitwa na fasihi andishi kama Usasa na Usasaleo, katika fasihi simulizi ni Ukale na Ukalejadi katika fasihi simulizi ya Mwafrika. Foley (1995) anasisitiza zaidi sifa ya usimulizi katika matini pamoja na mpangilio maalum wa mistari. Vilevile, anafafanua kuwa matini simulizi inapaswa kuwasilishwa kimistari kama ilivyotolewa na fanani katika utendaji wa fani ya usemaji. Uwasilishaji huu hujikita katika vipengele kama vile, uradidi, shada, kiimbo na matumizi ya jazanda kama inavyodhihirika katika utafiti wetu wa matapo katika fasihi simulizi. Mwisho, anasema kuwa, utafiti wa nyanjani ni wa lazima katika uchanganuzi wa fani ya usemaji, lakini sio matini simulizi iliyoandikwa. Hali hii ndiyo inayodhihirisha hali halisi kupitia kwa matapo mbalimbali hususan nyimbo katika utafiti huu. Kwa hivyo, fanani ni muhimu sana katika kazi hii kwa vile maana; yaani Isimu Amali hubainishwa kwa kuchunguza maana ya ishara na maneno katika muktadha wa matumizi ndani ya mawasiliano, yaani ishara na mtumiaji wake katika jamii husika kama namna ambavyo mifano katika kila tapo inavyojitokeza.

## HITIMISHO

Fasihi Simulizi ni taaluma ambayo hutendwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na vilevile haipatikani kwenye ombwe tupu bali husaidia katika ujenzi wa jamii kwa kuzingatia maadili, ujumbe, falsafa na jumla ya kazi inayohusika. Kwa hivyo, ni tukio linalofungamana na muktadha (mazingira) fulani wa kijamii na kutawaliwa na mwingiliano wa fanani, hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahali na wakati. Hivyo basi, haina budi kuingiliana na taaluma nyingine hususan dini. Isitoshe, matapo pia ni vijenzi vya fasihi hii.

Juhudi zifanywe ili tafiti nyingi zitekelezwe katika fasihi simulizi kwa ajili ya kuzua maendeleo faafu kijamii, kiuchumi na kisiasa katika Afrika Mashariki. Fasihi simulizi ipewe hadhi inayostahili. Tafiti ziendelezwe kwa kina kuhusu nadharia na jinsi zinavyoweza kutumika kuzua dhana mpya katika fasihi simulizi. Dhana za kisasa kama Teknolojia zitafitiwe katika fasihi.

## MAREJELEO

Abrams, M. H. A. (1993). *Glossary of Literary Terms.* New York: Holt, Reinehart and Winston.

Balisdya, N. (1991). *Shida*. Nairobi. Foundation Books.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa.* UK: Open Book Publishers CIC Limited. http://www..open book publishers. com

Foley, J. M. (1995). *The Singer of Tales in Performance*. Bloomington and Indianapolis.

Harvilahti, L. (2001) Subtrates and Registers: Trends in Ethnocultural Research, katika Wolf Knuts, U. na A. Kaivola-Bregenhoj. (Wah). Pathways: Uk 18-27 Turku)

Jamii ya Biblia ya Kenya na Tanzania (1997). *Biblia, Maandiko Matakatifu ya Mungu*. The Bible Societies of Kenya & Tanzania. Nairobi & Dodoma.

Kamusi ya Karne ya 21 (2014). *Kamusi ya Kiswahili yenye uketo zaidi katika karne hii*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Kahigi, K. & M. Mulokozi (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani* Yetu. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Kirumbi, P. S. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya.

Matei, A. K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa shule za upili.* Nairobi: Oxford University Press

M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi (Shule na vyuo).* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mrikaria, S. (2007). *Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya.* Swahili Forum 14: 197-2006.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam Printing Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948

Njogu, K., Momanyi, C., na Mathooko, M. (wah.) (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi: Twaweza Communication.

Ntarangwi, M. (2004). *The Challenges of Education and Development in Post Colonial Kenya.* Africa Development.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa. Towards a Poetics of the Oral Performance*. New York: Columbia University Press. http://www.jstor.org/discover/10.2307/3818229/iud 3/7/2017

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publishers.

Wanjala, S. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Wanjala, S. F, (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa*. Tasnifu ya Uzamifu. Nairobi: Ndaki ya Kenyatta.

Wanjala, S. F. (2020). *Safina ya Utafiti wa Fasihi Simulizi*. Kakamega: Elgon Epitome Publishers Ltd.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.